Washington State Department of CHILDREN, YOUTH & FAMILIES

# Idhini
## Authorization

**IDHINI YA KUFICHUA REKODI ZA IDARA YA WATOTO, VIJANA, NA FAMILIA (DCYF) ZA:**

| JINA, LA MWISHO | LA KWANZA | LA KATIKATI | TAREHE YA KUZALIWA |
|---|---|---|---|
| | | | |

| Taarifa ifuatayo inaweza kusaidia kutafuta rekodi | MAJINA YA ZAMANI |
|---|---|

| NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MTEJA | NAMBARI NYINGINE YA UTAMBULISHO | TAREHE YA HUDUMA | ENEO LA HUDUMA |
|---|---|---|---|
| | | | |

**FICHUA KWA:**

| JINA, LA MWISHO | LA KWANZA | LA KATIKATI | CHEO |
|---|---|---|---|
| | | | |

SHIRIKA AU JINA LA BIASHARA KAMA INAHUSIKA

| ANWANI | MJI | JIMBO | MSIMBO WA POSTA |
|---|---|---|---|
| | | | |

| NAMBARI YA SIMU (JUMUISHA MSIMBO WA ENEO) | NAMBARI YA NUKUSHI (JUMUISHA MSIMBO WA ENEO) | ANWANI YA BARUA PEPE |
|---|---|---|
| | | |

SABABU ZA UFICHUZI (SI LAZIMA)

**IDHINI:**

VYANZO: Naidhinisha programu zifuatazo za DCYF kufichua au kutoa ufikio wa taarifa za siri kuhusu mimi kama ilivyoainishwa hapo chini. Taarifa inaweza kutolewa kwa maneno au kwa uhamishaji wa data ya kompyuta, barua, nukushi au kuwasilishwa kwa mkono.

Programu zifuatazo pekee (tiki zote zinazohusika):

- ☐ Programu za Kurekebisha Tabia kwa Vijana
- ☐ Rekodi zangu zote kama mteja
- ☐ Rekodi nyingine za siri zinazoshikiliwa na vitengo vya DCYF zilizowekea alama hapo juu
- ☐ Rekodi kwenye orodha iliyoambatanishwa
- ☐ Taarifa binafsi zilizopo kwenye rekodi zinazohusiana na ajira
- ☐ Rekodi zifuatazo tu: Nyingine:
- ☐ Vitengo vyote vya Idara ya Watoto, Vijana, na Familia (DCYF)

<u>REKODI</u>: Naidhinisha rekodi zifuatazo za DCYF kufichuliwa:

- ☐ Rekodi za mteja zinazoshikiliwa na vitengo vya DCYF zilizowekea alama hapo juu
- ☐ Rekodi zangu zote kama mteja
- ☐ Rekodi nyingine za siri zinazoshikiliwa na vitengo vya DCYF zilizowekea alama hapo juu
- ☐ Rekodi kwenye orodha iliyoambatanishwa
- ☐ Taarifa binafsi zilizopo kwenye rekodi zinazohusiana na ajira
- ☐ Rekodi zifuatazo tu:

Nataka kuweka kikomo kwa rekodi zinazopaswa kufichuliwa kama ifuatavyo (kwa tarehe, aina ya rekodi, n.k.):

**TAFADHALI ZINGATIA: Ikiwa mteja wako au rekodi nyingine za siri zinajumuisha yoyote ya taarifa ifuatayo, unapaswa pia kujaza sehemu ya hapo chini ili kuruhusu ufichuzi wa rekodi hizi.**

<u>REKODI MAALUM</u>: Natoa ruhusa ya kufichua taarifa zifuatazo zilizopo kwenye rekodi za DCYF (tiki zote zinazohusika):

- ☐ Rekodi za majibu ya upimaji, uchunguzi au matibabu ya VVU/UKIMWI na Magonjwa ya Zinaa (RCW 70.02.220)
- ☐ Rekodi za afya ya akili (RCW 70.02.230 au 240)
- ☐ Rekodi za Utegemezi wa Kemikali (CD) (42 CFR Sehemu ya 2)

- Ruhusa hii ni halali kwa siku 180 au ☐ mpaka ____________________ (tarehe au tukio, ikiwa haitatikiwa, itakuwa siku 180).
- Naweza kubatilisha au kuondoa ruhusa yangu kwa maandishi wakati wowote, lakini hatua hiyo haitaathiri taarifa iliyokwisha kutolewa tayari.
- Naelewa kwamba rekodi zangu zinaweza kutolindwa tena chini ya sheria zinazohusika kwa DCYF baada ya kuwa zimeshatolewa.
- Nakala ya fomu hii ni halali kutoa ruhusa yangu ya kufichua rekodi hizi. DCYF inaweza kutoza ada ili kutoa nakala za rekodi zake.

| IMEIDHINISHWA NA (SAINI) | TAREHE ILIYOSAINIWA | NAMBARI YA SIMU (JUMUISHA MSIMBO WA ENEO) |
|---|---|---|
| | | |

| ANDIKA JINA | SHAHIDI/MTHIBITISHAJI (SAINI NA ANDIKA JINA, KAMA INAHUSIKA) |
|---|---|
| | |

Iwapo mimi si mhusika wa rekodi hizi, nimeidhinishwa kusaini kwa sababu mimi ni: (ambatisha uthibitisho wa kupewa mamlaka)
☐ Mzazi wa mtoto mdogo ☐ Mlezi Halali ☐ Mwakilishi Binafsi ☐ Mwingine:

**<u>Notisi kwa wale wanaopokea taarifa</u>: Kama rekodi hizi zinajumuisha taarifa kuhusu VVU, Magonjwa ya Zinaa, au matumizi mabaya ya pombe au dawa za kulevya, huwezi kufichua zaidi taarifa hizo kwa mujibu wa sheria ya serikali kuu na jimbo bila ya ruhusa mahsusi ya mhusika na kukidhi matakwa mahsusi ya kisheria.**

## MAELEKEZO YA UJAZAJI WA FOMU YA IDHINI

**Dhumuni:** Unapaswa kutumia fomu hii pale unapotaka DCYF kuwa na uwezo wa kufichua taarifa za siri zinazohusu wewe kwa mtu mwingine (akiwemo wakili, mtunga-sheria, au ndugu). Unaweza kutoa ruhusa ya kufichua rekodi zote za siri ilizonazo DCYF kuhusu wewe au unaweza kuweka kikomo cha ruhusa yako kwa rekodi mahsusi au vitengo vya shirika. Fomu hii pia itairuhusu DCYF kujadili suala lako kwa maneno pamoja na mtu unayemuidhinisha.

**Notisi kwa Wateja:** Taarifa nyingi za wateja ilizonazo DCYF ni za siri na hazitafichuliwa kwa wengine isipokuwa kama umeruhusu au kama ufichuzi unaruhusiwa na sheria. Baada ya DCYF kufichua taarifa zako za siri, tafadhali tambua kwamba mpokeaji anaweza kutolinda rekodi zako kwa mujibu wa ya sheria zile zile zinazohusika kwa DCYF. DCYF haiwezi kukunyima mafao kama hutosaini fomu hii ya kuruhusu fichuzi kwa DCYF isipokuwa kama idhini yako inahitajika ili kubaini ustahili. Kwa taarifa kuhusu jinsi vipengele vya huduma ya afya vya DCYF vinavyosimamiwa na HIPAA, kushirikisha taarifa zinazolindwa za afya na haki zako za ufaragha, tafadhali wasiliana na DCYF Notisi ya Taratibu za Ufaragha kupitia www.DCYF.wa.gov au muulize mtu aliyekupa fomu hii. Unaweza kupata nakala ya fomu hii.

**Matumizi:** Unaweza kujaza fomu hii kielektroniki au kwa mkono. Tumia kibambo tabo (Tab key) katika kompyuta ili kuhama kati ya uga. Fomu nyingine inapaswa kujazwa kwa kila mtu ambaye rekodi zake zinaombwa, wakiwemo watoto. “Wewe” inarejelea mhusika wa rekodi.

**Sehemu za Fomu:**

**UTAMBULISHO WA MHUSIKA WA REKODI:**

- Jina: Andika jina lako kamili au jina la mtu ambaye rekodi zake zinaombwa kama unamwakilisha mtu mwingine.
- Tarehe ya Kuzaliwa: Tafadhali jumuisha taarifa hii inayohitajika ili kumtambua mteja kati ya watu wanaofanana majina.

**TAARIFA ZA HIARI ili kusaidia kutafuta rekodi:**

- Majina ya zamani: Jumuisha majina mengine yoyote ambayo yamewahi kutumika wakati wa kupokea mafao au huduma.
- Nambari ya utambulisho wa mteja: Andika nambari yoyote ambayo DCYF inaweza kuwa iliitoa.
- Nambari nyingine ya utambulisho: Jumuisha kitambulisho kingine chochote kinachoweza kusaidia kupata rekodi za DCYF. Andika nambari ya huduma za kijamii (SSN) kama ni lazima.
- Tarehe na eneo la huduma: Andika taarifa hii ili kuisaidia DCYF kutambua na kupata rekodi unazotaka zifichuliwe.

**MTU ANAYEPOKEA REKODI:**

- Utambulisho: Tafadhali jaza sehemu hii kikamilifu kadri iwezekanavyo ili tuweze kuwasiliana na mtu au shirika litakalopata ufikio wa taarifa zako za siri.
- Sababu za Ufichuzi: Taarifa hii inahitajika kabla DCYF kuweza kushirikisha rekodi za dawa za kulevya na pombe au afya ya akili. Kama hutajaza sehemu hii, DCYF itaandika sababu za ufichuzi kuwa ni kwa ombi lako.

**IDHINI:**

- Vitengo vya DCYF: Tafadhali weka alama ama vitengo vya DCYF unavyotaka kufichua rekodi au weka alama katika kisanduku cha chini cha sehemu hii kama unataka kutoa ufikio kwa rekodi zozote ambazo DCYF inazo kuhusu wewe. Andika jina la programu katika “Nyingine” kama haipo kwenye orodha.
- Taarifa zinazofichuliwa: Ainisha ni rekodi gani unazotaka zifichuliwe. Unaweza kuruhusu ufichuzi kamili au sehemu ya mteja wako wa DCYF au rekodi nyingine za siri. Unaweza pia kuweka kikomo cha ufichuzi kwa rekodi za mteja zinazoshikiliwa tu na vitengo vya shirika vilivyowekewa alama hapo juu, au kwa rekodi mahsusi zilizoorodheshwa kwenye fomu hii au kwenye kiambatisho unachosaini. Kama kuna ukomo wowote kwenye rekodi unazotaka zifichuliwe, ama orodhesha rekodi mahsusi au elezea ukomo huo, kama vile kwa tarehe ya huduma au aina ya rekodi.
- Rekodi zinazozuiliwa: Ikiwa rekodi yoyote inajumuisha taarifa kuhusu kupima au matibabu ya VVU/UKIMWI au Magonjwa ya Zinaa, matibabu ya afya ya akili, au huduma za dawa za kulevya na pombe, unapaswa kutiki kila kipengele ili kuruhusu DCYF kufichua rekodi hizi. Unahitajika kujaza fomu nyingine ili kuidhinisha ufichuzi wa maelezo ya matibabu ya kisaikolojia (45 CFR 164.508(b) (3) (ii)).
- Uhalali: Fomu hii ni halali kwa kutoa ufikio wa taarifa zinazoshikiliwa kwa sasa na DCYF Ruhusa yako inaisha muda wake siku 180 baada ya kusaini au katika tarehe au tukio lingine lolote ulilolianadika. Kama hutaandika tarehe, idhini hii itakuwa halali kwa siku 180. Unaweza kubatilisha mamlaka ya kuachia rekodi kwa maandishi wakati wowote lakini itakuwa imechelewa kurejesha taarifa zilizotolewa tayari.
- Gharama: Sheria ya rekodi za umma katika RCW 42.56.120 na WAC 388-01-080 inairuhusu DCYF kutoza ada kwa ajili ya nakala za rekodi pamoja na gharama za utumaji. Hospitali za jimbo na vituo vya afya wanaweza kutoza ada kwa rekodi za wagonjwa kwa mujibu wa Sura ya 70.02 RCW.

**SAINI:**

- Kama wewe ndiwe mhusika wa rekodi hizi, saini na pia andika au chapa jina lako hapo chini. Weka tarehe uliyosaini na nambari yako ya simu au mawasiliano.
- Kama unamsainia mtu mwingine, ainisha kwa nini unaweza kufanya hivyo kwenye mstari wa mwisho na ambatisha nakala ya amri ya mahakama au nyaraka nyinyine inayokupa mamlaka ya kisheria. Watoto pia wanapaswa kusaini ili kutoa ruhusa ya kufichua rekodi zao za siri kama wamefikisha umri wa kutoa ridhaa (miaka 13 kwa huduma za afya ya akili na dawa za kulevya na pombe; miaka 14 kwa taarifa za VVU/UKIMWI au Magonjwa mengine ya Zinaa; umri wowote kwa kupanga uzazi na kutoa mimba; miaka 18 kwa afya au rekodi nyingine).

Shahidi au mthibitishaji: Shahidi au mthibitishaji anaweza kuhitajika ili kuthibitisha utambulisho wako kama hutawasilisha fomu hii wewe binafsi au kama programu husika inahitaji uthibitisho. Mtu huyu anapaswa kusaini na kuandika jina lake.

**NOTISI KWA DCYF:** Kama rekodi hizi zinajumuisha taarifa za VVU au Magonjwa ya Zinaa, DCYF inapaswa kuwataarifu wapokeaji kwamba taarifa hizi ni za siri na kwamba hawapaswi kuzifichua zaidi rekodi hizi bila ya idhini mahsusi kwa mujibu wa RCW 70.02.300. Kama DCYF itatuma nakala za rekodi zinazohusiana na huduma za dawa za kulevya na pombe chini ya idhini hii, DCYF lazima ijumuishe tamko lifuatalo wakati wa kufichua taarifa kwa mujibu wa 42 CFR 2.32:

Taarifa hii imefichuliwa kwako kutoka kwenye rekodi zinazolindwa na kanuni za usiri za Serikali Kuu (42 CFR sehemu ya 2). Kanuni za Serikali Kuu zinakukataza kufichua zaidi taarifa hii isipokuwa kama ufichuo huo wa ziada umeruhusiwa waziwazi kwenye ridhaa ya maandishi ya mhusika au vinginevyo kama inavyoruhusiwa na 42 CFR sehemu ya 2. Idhini ya kawaida kwa ajili ya kuachilia taarifa za kitiba au nyingine HAITOSHI kwa ajili ya dhumuni hili. Kanuni za Serikali Kuu zinazuia matumizi yoyote ya taarifa husika ili kuchunguza uhalifu au kumshitaki mgonjwa yeyote anayetumia vibaya pombe au dawa za kulevya.